


# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Simu : (027) 2503538/ 2507928  
Nukushi: (027) 2505973  
Barua pepe: [rbcarusha@pccb.go.tz](mailto:rbcarusha@pccb.go.tz)  
Wavuti : [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

---

#### **TAKUKURU ARUSHA YAOKOA ZAIDI YA SHILINGI MILIONI 43 ZA KIKUNDI CHA IMANI ZILIZODAIWA KUPOTEA KIMAZINGIRA**

TAKUKURU Mkoa wa Arusha, Leo Februari 21, 2020 itakabidhi jumla ya kiasi cha fedha cha shs. 43,328,000/- kwa wanachama wa kikundi (kikoba) cha Imani kilichopo mtaa wa Ngusero Jijini Arusha. Fedha hizi ni zile ambazo mnamo tarehe 08.12.2019 zilidaiwa kupotea ***kimazingara*** kutoka kwenye sanduku lililokuwa linatumika kuhifadhia fedha hizo.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Arusha umebaini kwamba, Fedha hizo ambazo hapo awali zilidaiwa kupotea, ilikuwa ni michango ya wanachama wa kikundi hicho wapatao ishirini na nane (28) ambao walianza kujiwekea akiba yao kila wiki tangu mwaka 2014. Baada ya miaka mitano ya kujiwekea akiba ambayo pia walikuwa wanakopeshana na kuzalisha faida, mnamo tarehe 08.12.2019 walipanga kuvunja kasha walilokuwa wanahifadhia fedha hizo kwa lengo la kugawana akiba na faida iliyokuwa imepatikana.

Kinyume na matarajio ya wananchama hao waliokuwa wamekutana nyumbani kwa mweka hazina wa kikundi hicho, waliwatangaziwa na viongozi wao kuwa fedha kiasi cha Tsh 39,000,000/= zilikuwa hazionekani katika sanduku hilo.

Baada ya kupokea malalamiko haya ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Arusha ilifanya uchunguzi na kubaini kwamba edha hizo zilikuwa zimefanyiwa ubadhirifu na viongozi wa kikundi hicho cha imani ambao ni Mwenyekiti, Katibu, Mweka Hazina, Mweka Hazina Msaidizi na Watunza funguo za sanduku. Uchunguzi ulichukua hatua ya kumwagiza Afisa Maendeleo ya Jamii na Mhasibu wa kata ya OSUNYAI JR mahali kilipo kikundi cha Imani, kufanya ukaguzi wa fedha zote za kikundi hicho ili kubaini kiasi halisi ambacho kilikuwa kimepotea. Mkaguzi huyo alibaini upotevu wa Zaidi ya shilingi milioni 44 za kikundi cha Imani tofauti na ilivyokuwa imeelezwa hapo awali. Baada ya taarifa hiyo ya mkaguzi, uchunguzi uliwapa muda Viongozi wote wa kikundi cha Imani, kuhakikisha kuwa wanatafuta na kurejesha fedha ambazo Ukaguzi ulibaini walizifanyia ubadhirifu.

Kwa utaratibu uliokuwa umewekwa, Uchunguzi ulifanikiwa kukusanya jumla ya fedha Tsh 43,328,000/= ambapo kati ya hizo Tsh 23,973,000/= zikiwa ni fedha taslimu walizorejesha baadhi ya Viongozi hao na mikopo ambayo iliyokuwa kwa baadhi ya wanachama waliokuwa wakidaiwa. Kiasi cha Tsh 19,355,000/= ni fedha za hisa ambazo baadhi ya Viongozi waliridhia wakatwe hisa zao ili kulipa deni hilo la fedha za kikundi cha Imani

Jumla ya fedha taslimu inayopaswa kurejeshwa kwa wanachama wa kikundi cha Imani wanaodai mgao wao ni Tshs. 27,855,000/- na fedha taslimu ambazo zimekusanywa ni Tshs. 23,973,000/- hivyo kuwepo kwa upungufu wa Tshs. 3,882,000/- ambazo bado hazijalipwa na viongozi wawili. Ili kuwawezesha wanachama wa kikundi cha Imani wasiokuwa na hatia kupata fedha zao, ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Arusha leo itamrejeshea kila mwanachama anaedai, asilimia

themanini na tano(85%) ya madai yake na fedha nyingine iliyobaki, wanachama hao watapewa baada ya viongozi waliobaki kuziwasilisha TAKUKURU.

TAKUKURU Mkoa wa Arusha tunatoa wito kwa jamii kuacha tama na ubinafsi wa fedha wanazokuwa wamekubaliana kuchangishana kwa lengo la kujiboreshea Maisha yao. Aidha pia wanaaswa kufuata sheria na taratibu

Katika uendeshaji wa vikundi hivyo ikiwemo utunzaji mzuri wa kumbukumbu, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mahesabu yao na kuhakikisha kuwa fedha wanazozikusanya zinahifadhiwa benki ambako ni sehemu salama.

**Imetolewana:**

**FRIDA WIKESI,**

**MKUU WA TAKUKURU MKOA WA ARUSHA**

**JANUARI 21, 2020**

---